**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

## BODI YA KAHAWA TANZANIA

# TANGAZO

## UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2025/2026

## UTANGULIZI

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anawatangazia ufunguzi wa msimu mpya wa ununuzi wa kahawa kwa mwaka 2025/2026. Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 (1) ya Kanuni za Kahawa 2013. Tarehe za ufunguzi wa msimu na kuanza kwa ununuzi wa kahawa katika kanda za uzalishaji kahawa ni kama ifuatavyo;

| Na. | Kanda | Mkoa | Tarehe ya Ufunguzi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kigoma | Kigoma, Katavi | 14 April, 2025 |
| 2. | Mara | Mara, Mwanza | 14 Aprili, 2025 |
| 3. | Kagera | Kagera | 1 Mei, 2025 |
| 4. | Mbeya, Songwe | Mbeya, Songwe | 15 Juni, 2025 |
| 5. | Ruvuma | Ruvuma, Iringa, Njombe | 1 Julai, 2025 |
| 6. | Kaskazini | Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga | 1 Julai, 2025 |

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MSIMU HUU 2025/2026

1. Bodi inatoa taarifa kuwa kuanzia msimu huu wa kahawa 2025/2026 Bodi itaanza kuendesha minada ya kahawa ghafi ya kahawa za arabika laini (Arabica Parchment Coffee). Utaratibu huu mpya unaondoa utaratibu wa mauzo ya kahawa ghafi ya Arabika kwa njia ya kuingia mikataba ya mauzo kati ya AMCOS na wanunuzi wa kahawa. Taratibu za uendeshaji wa minada hii zitatolewa kwenye mwongozo wa masoko utakaotolewa na Bodi kwa mujibu wa sheria.
2. Katika kanda zote za uzalishaji wa kahawa ukusanyaji na uuzaji wa kahawa utafanyika kupitia AMCOS, vyama vikuu vya ushirika vitakuwa na wajibu wa kuratibu makusanyo na uuzaji wa kahawa na iwapo vyama vikuu vitakuwa na nia ya kununua kahawa vitatakiwa kufanya hivyo kwa kufungua Kampuni tanzu na kushindana na wanunuzi wengine kununua kahawa iliyokusanywa na vyama vya msingi.

3. Bodi inashauri Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa kutoa vibali vya kununua kahawa kwa wanunuzi wenye nia ya kununua kahawa kwenye Halmashauri zao mapema kabla ya tarehe ya kuanza msimu ikiwa ni moja ya masharti yaliyotolewa ili kupata leseni ya ununuzi wa kahawa kwa mujibu wa Jedwali la Tatu la Kanuni za Kahawa 2013. Endapo Halmashauri itachelewesha au kukataa kutoa kibali pasipo sababu za msingi, Bodi itatoa leseni kwa mujibu wa Kanuni ya 26 (2) ya Kanuni za Kahawa, 2013.

4. Maombi ya leseni zote mpya na maombi ya kuhuisha (renewal) leseni kwa wanunuzi wa kahawa yatafanyika kwa njia ya mtandao katika mfumo wa kwa **e-Kilimo** kufuata kiungo cha **https://portal.kilimo.go.tz**

5. Vyama vyote vya msingi vinatakiwa kuzingatia tarehe hizi za ufunguzi wa msimu na kufanya maandalizi muhimu ya kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima na kuitayarisha kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya kahawa. Wito huu unatolewa ili vyama vya msingi vianze kusanya kahawa inapokuwa tayari na kuwezesha kahawa hiyo kuuzwa na kulipwa fedha zao mapema.

6. Bodi ya Kahawa Tanzania itaanza kuendesha minada ya kahawa ghafi katika mkoa wa Kagera (Dry cherry Auction) na mnada wa kahawa ghafi ya Arabika (Parchment Coffee Auction) katika maeneo mengine mara tu itakapopokea taarifa za uwepo wa kiasi cha kutosha cha kahawa kuendesha mnada kutoka kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi. Pia Bodi itaanza kuendesha minada ya kahawa safi baada ya kupokea taarifa za uwepo wa kahawa na sampuli kutoka viwanda vya kukobolea kahawa.

7. Vyama vya Ushirika vya Msingi vitapaswa kuhakikisha kuwa akaunti zao za malipo zipo hai (zinafanya kazi) ili kuwezesha zoezi la uuzaji wa kahawa na malipo kufanyika mapema na kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya fedha za wakulima.

8. Vyama vya Ushirika vya Msingi vitakavyouza kahawa mnadani vitahuisha vibali vyao au kuomba vibali vipya kwa kujaza fomu maalum. Fomu hizo zinapatikana katika tovuti ya Bodi ya Kahawa, ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa, viwanda vya kukobolea kahawa na ofisi za Vyama Vikuu vya Ushirika. Pale itakapobidi Vyama hivi vitasaidiwa kuomba vibali katika mfumo wa e-Kilimo na maofisa waliopo kwenye ofisi za kanda za Bodi ya Kahawa, Viwanda vya kukobolea kahawa na Vyama Vikuu vya Ushirika.

9. Vyama vya Ushirika vihakikishe kuwa mitambo ya kuchakata kahawa (CPU) iliyoko katika maeneo yao inatumika na inafunguliwa mara tu kahawa zinapokuwa tayari na pia kumuweka mtunza ubora wa kahawa katika CPU ili kufanikisha lengo la Serikali la kuongeza ubora wa kahawa na bei ya mkulima. Aidha makampuni yenye nia ya kushirikiana na vyama vya ushirika kuendesha CPU yanatakiwa kuingia makubaliano na vyama husika na kuomba leseni ya kuendesha mitambo ya kuchakata kahawa (Ripe Cherry Prossing Llisence).

10. Makampuni binafsi yaliyoingia makubaliano ya kilimo cha mkataba na Vyama vya Ushirika wanatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa makubaliano yao kwa ajili ya tathimini na ufuatiliaji kwa mujibu wa Kanuni ya 59 ya Kanuni za Tasnia ya Kahawa 2013 kabla ya makubaliano ya mauziano ya kahawa kufanyika. Bodi haitasajili makubaliano ya kilimo cha mkataba wakati wa mauzo ya kahawa

11. Utaratibu wa ukusanyaji, uuzaji na ununuzi wa kahawa ghafi (Dry Cherry) kupitia Vyama vya Msingi na pia uendeshaji wa minada ya kahawa ghafi katika Mkoa wa Kagera utafanyika kama ilivyofafanuliwa katika Mwongozo Na. 1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Kahawa kwa Msimu 2023/2024.

Primus O. Kimaryo

**<u>MKURUGENZI MKUU</u>**

**BODI YA KAHAWA TANZANIA**

**S. L. P. 732 Moshi, Simu: 027-2752324**

**Barua pepe: info@coffee.go.tz; Tovuti: www.coffee.go.tz**